MSIMBO WA KOZI: KSW 101

JINA LA KOZI: UTANGULIZI WA FASIHI NA NADHARIA

SHAHADA YA ELIMU KATIKA LUGHA NA UTAWALA (BELM)

Mhadhiri wa Kozi: FULUGE, Adria

Mhadhara wa Pili

Dhima ya Fasihi

Wahakiki mbalimbali hufafanua dhima ya fasihi kwa njia mbalimbali. Wanataaluma kama vile Aristotle, Immanuel Kant, T. Gautier pamoja na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kama vile John Ramadhani, E. Kezilahabi, N. Balisidya, M.M. Mulokozi wamefafanua dhima ya fasihi.

Swali la semina: Je, hawa ni akina nani na wamesema nini kuhusu dhima ya fasihi: Aristotle, Immanuel Kant, T. Gautier?

Aristotle (1958:xiv) aliipa fasihi ya wakati wake dhima tatu:

- **kuburudisha** (msomaji/msikilizaji wa kazi ya fasihi huburudika: husisimka kimwili na kiakili na kuvutiwa kihisia na kazi ya fasihi)
- **kujenga tabia** (mafunzo na mifano bora ya matendo ya kuigwa katika kazi ya fasihi huweza kujenga tabia njema)
- **kustarehesha** (kwa Aristotle, ni hali ya kupumzika baada ya kazi na burudani)

Wahakiki wa Ulaya waliokuja baada ya Aristotle waligawanyika katika makundi mawili kuhusu dhima ya fasihi. **Kundi la kwanza**, na lililo kubwa zaidi, lilidai kuwa **fasihi ina dhima muhimu ya kijamii; fasihi ni sanaa "tamu na tumizi"**. Katika karne ya 19 na 20, wahakiki wa Kimarx waliendeleza mtazamo huu kwa kuihusisha zaidi dhima/kazi ya fasihi na vuguvugu halisi la watu au makundi ya watu katika muktadha mahsusi, kama vile:

- kuburudisha
- kuelimisha
- kujenga tabia
- kuhifadhi amali (matendo, kazi, mazoea) za jamii
- kuonyesha ukweli kuhusu maisha

- kuhifadhi lugha
- kuendeleza harakati za jamii dhidi ya mazingira
- kujenga utaifa

Kundi la pili la wahakiki wa Ulaya wa dhima ya fasihi walidai kuwa **“sanaa ni kwa ajili ya sanaa tu”** (*l’art pour l’art*; *art for art’s sake*).

- sanaa inajitosheleza yenyewe
- haipaswi kuhusishwa na mambo yaliyo nje ya sanaa (k.v. maadili, siasa)
- jambo muhimu katika sanaa ni uzuri/ujumi wake tu

Hivyo basi, walidai, fasihi haina au haipaswi kuhusishwa na dhima yoyote ya kijamii (**Immanuel Kant**, mwanafalsafa Mdachi, 1724-1804; ikaendelezwa na **T. Gautier**, katika dibaji ya riwaya *Mademoiselle de Maupin*, 1835; na watunzi wengine wa Marekani na Uingereza).

Mtazamo huu wa kundi la pili haujapata kuathiri sana nadharia ya fasihi ya Kiswahili au hata ya Kiafrika. Wahakiki wa fasihi ya Kiswahili wanakubaliana na dhima karibu zote zilizotajwa na wahakiki wa Ulaya, isipokuwa ile ya “sanaa kwa ajili ya sanaa tu”. Hata hivyo, wao wanapozungumzia dhima za fasihi, wamekuwa wakisisitiza zaidi vipengele vifuatavyo:

- **kuasa**: fasihi ina dhima ya malezi kwa watoto na maonyo kwa watu wazima
- **kufunza** au kuelimisha
- **ukombozi**: fasihi imsaidie Mwafrika kujikomboa kitaifa, kisiasa, kiuchumi, kitabaka, n.k. (kazi za akina Ngugi wa Thiong’o, A.E. Musiba, Ben Mtobwa, n.k.)
- **ujenzi wa utaifa**: fasihi isaidie kuleta umoja na mshikamano wa kitaifa
- **kukuza na kuhifadhi lugha**: limeegemea zaidi upande wa ushairi
- **kuhifadhi na kurithisha amali za jamii**.

Tunapojadili dhima ya fasihi, hatuna budi kuzingatia dhana mbili muhimu: dhana ya **tabaka** na dhana ya **itikadi**.

Tabaka ni makundi ya watu yanayounganishwa na *uhusiano wao* na *njia za kuzalisha mali*, na *mfumo wa mamlaka*, katika jamii.

Itikadi, tunaweza kusema, ni namna yale tuyasemayo na kuyaamini yanavyohusiana na mfumo wa mamlaka na mahusiano ya kiutawala ya jamii tunayoishi.

Ili kuelewa vizuri uhusiano uliopo kati ya fasihi na dhana za tabaka na itikadi, **ni muhimu kwanza kukumbuka kuwa fasihi yoyote ile hufungamana na muktadha maalumu**.

Muktadha ni mazingira ya kijiografia, kiutamaduni, kiuchumi, kisiasa, na kiwakati. **Kila kazi ya fasihi hufungamana na muktadha ulioizaa**.

Pili, fasihi ni namna maalumu ya kuuelewa na kuusawiri ulimwengu kulingana na hali ya maendeleo ya jamii husika

- inadhihirisha aina fulani ya urazini (maelezo ya kanuni, missing au sababu; sababu za msingi za kufanya jambo) na utambuzi wa hali ya maisha alio nao mtunzi na anaowawakilisha.
- hutumia lugha, maumbo, mbinu, ufundi, na mitindo inayopatikana na inayowezekana katika jamii inayoizua
- hivyo, maisha halisi ndiyo msingi na ndiyo yanayozaa fasihi

Tatu, zipo jamii za aina mbili:

- jamii zenye usawa na mshikamano
- jamii zenye mgawanyiko wa makundi.

Jamii zenye usawa na mshikamano hazijagawanyika katika makundi au matabaka yenye uhasama; yaani, **jamii za kiujima**.

- fasihi yake mara nyingi huonyesha hali ya mshikamano wa jamii hizo
- husisitiza usawa, ushirikiano na umoja katika kukabiliana na mazingira au maadui wa jamii
- hukemea tabia ya ubinafsi, uchoyo, majivuno (*Kusadikika*, *Mabepari wa Venisi*)
- huendeleza itikadi ya kiujima ya jamii hiyo
- hadithi nyingi za kimapokeo (ngano) (*Hapo zamani za kale* ...)

Jamii zenye mgawanyiko wa makundi, kwa mfano matabaka au *castes* (makundi ya watu wenye kufanya kazi ya aina moja kijadi na ambayo hayaingiliani kijamii, kindoa, n.k.)

- mahusiano ya watu katika jamii hizo hutawaliwa na mgawanyiko huo
- mara nyingi mgawanyiko huo hujengwa katika umilikaji wa raslimali za jamii
- kuna mgawanyo mbaya wa mali ya jamii
- mamlaka za utawala mara nyingi hutokana na matabaka yanayomiliki uchumi
- dhima ya fasihi huonyesha mgawanyiko huo uliopo: fasihi huweza kulinda maslahi ya wenye mali (mfano, filamu za akina Chuck Norris), au kuipinga itikadi hiyo na kuchukua msimamo wa tabaka la chini (Bertolt Brecht)

Hivyo basi, dhima ya jumla ya fasihi ni:

kusawiri kisanaa hali ya mwanadamu, mazingira yake, uhusiano wake na mazingira hayo, mahusiano yake ya kijamii, na hisia na mawazo yake kwa lengo la kuelewesha, kubadilisha, au kuonyesha tu hali ilivyo.

Kwa ufafanuzi huo, dhima ya fasihi inagawanyika katika maeneo yafuatayo:

- itikadi
- uchumi
- utamaduni
- siasa
- falsafa

Dhima hizi huingiliana na mara nyingi huweza kutendwa na kazi ileile moja.

1. **Dhima ya fasihi kiitikadi**
   - hutegemea muktadha wa jamii husika
   - hutegemea pia nafasi ya mtunzi katika jamii hiyo na msimamo wake kuhusu migogoro na matatizo ya wakati wake
   - fasihi yaweza kuwa na dhima ya kueneza na kuendeleza itikadi ya tabaka tawala (*Mashimo ya Mfalme Sulemani*, *Uhuru wa Watumwa* vilitetea ukoloni)
   - jamii ya kitabaka na ya kijumuiya zinaweza kuwa na itikadi zinazopingana; kazi za fasihi huakisi vilevile hali hii. (“Kwetu ni kwao kwa Nini”, Saadan Kandoro; “Nikizipata Bunduki”, Seif Khatibu).

2. **Dhima ya fasihi kiuchumi**
   - dhima ya fasihi katika uchumi huonekana zaidi katika fasihi simulizi, hasa nyimbo za kazi
   - hutungwa ili ziimbwe wakati wa kazi ngumu (kulima, kuvua samaki, kuwinda, n.k.)
   - husaidia kuchapusha kazi (kuharakisha kazi) na kuondoa uchovu
   - katika uchumi wa kibepari, dhima ya fasihi huchomoza mambo mawili:

- kuburudisha wafanyakazi baada ya kazi ngumu (kuimba, kusoma riwaya, kuangalia mchezo wa kuigiza, sinema)
- kuwezesha wahusika (watunzi, makampuni ya kurekodi, makampuni ya wachapishaji, wapiga chapa na wauza vitabu) kupata fedha. Hivyo, fasihi ni shughuli ya uzalishaji mali na biashara.

3. Dhima ya fasihi kiutamaduni

Kiutamaduni, fasihi ina dhima ya:

- kuhifadhi na kurithisha amali za jamii (mila, desturi, mtindo wa maisha, imani, historia, visasili na visakale, urithi wa maarifa ya kijadi k.v. tiba, sayansi ya kilimo, mbinu za uwindaji, n.k.) (*The Gods Must be Crazy*)
- kuburudisha,
- kukuza, kudumisha na kuendeleza lugha,
- kuelimisha, kuasa na kurekebisha jamii (*Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka...; Kinjekitile*)

- nyimbo na visasili hutumika pia kukoleza shughuli za kijadi za kitamaduni k.v. ibada, matambiko, sherehe, n.k. Nyimbo huburudisha na kubeba ujumbe wa tukio.
- fasihi pendwa, k.v. masaibu na vituko vya ujambazi na uhalifu, humsisimua na kumpa msomaji imani kuwa naye anashiriki katika matukio ya kishujaa yanayosimuliwa
- malighafi ya fasihi ni lugha. Hukua na kupevuka kadri inavyotumiwa na kufinyangwa na watunzi wa riwaya, mashairi, nyimbo na tamthiliya (mf. vina, mizani, beti, mshororo, muwala, n.k).

4. Dhima ya fasihi kisiasa

- Fasihi imetumika mahali pengi kuendeleza au kuzuia harakati za kisiasa:
  - wakati wa harakati za kudai uhuru nyimbo zilitungwa kumsuta mkoloni
  - nyimbo za kutetea siasa ya ujamaa
  - “nyimbo za taifa”, “Tanzania, Tanzania” “Tazama Ramani”
- Hadithi na tamthiliya kueneza ujumbe wa kisiasa:
  - maigizo ya ngonjera (*Fataki la Wiki Hii* katika TBC1)
- Wakati wa vipindi vigumu vya zahama za kitaifa

- wakati wa vita ya Kagera

5. **Dhima ya fasihi kifalsafa**

Baadhi ya kazi za fasihi hujaribu kuelezea falsafa fulani kuhusu maisha.

- Kazi za aina hiyo hujaribu kuyachimbua masuala mazito kuhusu kuwepo kwa mwanadamu duniani na hatima yake.
- Hivyo, fasihi huwachochea wasomaji/wasikilizaji kutafakari masuala hayo kwa undani zaidi. (Mf. kazi za Kezilahabi: *Nagona*, *Mzingile*, *Karibu Ndani*; *Kiu* ya M.S. Mohamed).

Tamati

Tumeona kwamba fasihi ina dhima muhimu katika jamii, nazo zinaweza kuwa hasi au chanya kutegemeana na hali ya jamii yenyewe na msimamo alio nao mtunzi kuhusu migogoro ya jamii hiyo. Hivyo, dhima ya fasihi sharti ipimwe kwa kigezo cha jamii mahsusi.